



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KAHAMA



16/08/2022

TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI 2022

1.0 UTANGULIZI.

Ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Mapato na Matumizi kwa kipindi cha mwezi Julai, 2022 kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Taarifa hii inajumuisha mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani, Ruzuku toka Serikali Kuu inayoletwa kwa ajili ya mishahara ya watumishi, Matumizi Mengineyo (OC) na Fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo pamoja na matumizi yanayotokana na vyanzo hivyo.

2.0 MAPATO

kwa mwaka wa fedha 2022/2023 tunatarajia kupata mapato kutokana na vyanzo mbalimbali vikiwemo vyanzo vya ndani, Ruzuku toka Serikali Kuu na Wahisani kama ifuatavyo:

2.1 MAPATO KUTOKANA NA VYANZO VYA NDANI

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, tumejiwekea lengo la kukusanya jumla ya **Tshs.10,257,500,000.00 =**. Kwa kipindi cha mwezi Julai 2022 tulipanga kukusanya kiasi cha Tsh **952,856,661.00** ambapo jumla ya **Tshs. 602,136,349.66 zimekusanywa** ikiwa ni sawa na asilimia **63** ya lengo la makusanyo ya mwezi na asilimia **6** ya makusanyo ya Mwaka.

2.2 MAPATO YA RUZUKU YA MATUMIZI YA KAWAIDA

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Halmashauri inatarajia kupokea jumla ya **Tshs. 28,332,539,000.00 /=** ikiwa ni Ruzuku kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Fedha hizi zimegawanyika katika mchangano ufuatao:-

Mishahara	26,854,847,000.00
Matumizi Mengineyo.....	<u>1,477,692,000.00</u>
Jumla Kuu	<u>28,332,539,000.00</u>

Mapato ya Matumizi Mengineyo (OC)

Kwa kipindi cha mwezi Julai, 2022 kiasi cha **Tsh. 194,654,000.00** kimepokelewa kama mapato ya matumizi mengineyo.

2.3 MAPATO YA RUZUKU YA MIRADI YA MAENDELEO

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, tunatarajia kupokea jumla ya **Tshs. 11,855,535,900.00** ikiwa ni ruzuku kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mchanganuo wa ruzuku hiyo ni kama ifuatavyo:-

- Ruzuku toka Serikali Kuu Tshs. 3,593,733,000.00
- Ruzuku toka Wahisani Tshs 3,604,950,000.00
- Mchango wa Mapato ya Ndani (63%) Tshs. 4,656,852,900.00

JUMLA KUU TSHS. 11,855,535,900.00

Kwa kipindi cha Mwezi Julai 2022, Halmashauri imepokea Jumla ya **Tsh 156,356,644.60** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kutoka Serikali Kuu na Wahisani.

2.1 MATUMIZI KUTOKA MAPATO YA NDANI NA RUZUKU YA MATUMIZI YA KAWAIDA

Kutokana na mapato yaliyoonyeshwa hapo juu matumizi kwa mwezi Julai 2022 jumla ya Tsh 2,293,594,350 zilitumika katika kulipia Mishahara ya Watumishi.

Naomba kuwasilisha.


Anderson D. Msumba

MKURUGENZI

HALMASHAURI YA MANISPAA

KAHAMA

MUNICIPAL DIRECTOR
KAHAMA MUNICIPAL COUNCIL
P.O. Box 472
KAHAMA